

Picha na Emile Smith Dumont/ICRAF

# Misitu na Mabadiliko ya hali ya hewa inchini Kongo (FCCC)

## Maudhui

Misitu mikubwa mbalimbali ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ni yenye upekee na yenye thamani kubwa hata nje ya mipaka ya nchi hiyo. Inatunza viumbe anuai vyenye thamani kubwa ikiwemo hazina ya thamani ya kimaumbile inayochangia uhifadhi wa mazingira kwa dunia nzima.

Zaidi ya nusu ya DRC (takriban ekari milioni 125) ni misitu inayotoa kipato kwa theluthi mbili ya idadi ya watu wote. Misitu hii inawakilisha mazingira ya mfumo wa kiikolojia, ikiwa ni pamoja na ekari milioni 100 za msitu mnene wa unyevunyevu katika majimbo matatu katika Bonde la Kongo, misitu aina ya montane iliyopo Kivu Mashariki, eneo lenye idadi kubwa ya watu na jimbo la Ituri, Savanna, misitu yenye kustawi maeneo ya unyevunyevu na/au kando ya mito (gallery forest mosaics), Misitu ya wazi ya mbao kama vile Miombo katika mkoa wa Katanga .

Nchi hii pia ina kivutio cha Hifadhi ya Taifa ya Virunga, moja kati ya eneo lenye mchanganyiko mkubwa wa kibaiolojia duniani, nyumbani kwa masokwe watu walio katika hatari ya kutoweka aina ya sokwe wa milimani.

Kwa miaka mingi, migogoro ya kisiasa na kukosekana kwa maelewano kumezuia jitihada za kuvuna neema ya rasilimali ya misitu ili kuchangia katika maendeleo endelevu na usimamizi wa maliasili katika DRC. Tangu mwaka 2001, nchi imekuwa ikipiga hatua za kimaendeleo ikichangiwa na maboresho ya kisekta. Lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi kwa upande wa suala la kuchochea usimamizi na uhifadhi bora wa misitu hususan katika mabadiliko ya tabia nchi.

## Mradi

Misitu na Mabadiliko ya hali ya hewa inchini Kongo (FCCC) ni mradi ambao umeanzishwa ili kusaidia kutatua baadhi ya changamoto hizo. Kwa msaada toka Ushirika wa Umoja wa Ulaya katika Mabadiliko ya hali ya hewa duniani, Kituo cha Kimataifa kwa Utafiti wa Misitu (CIFOR) kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira ya DRC, Uhifadhi wa Mazigira na Utalii (MECNT) inafanya kazi na Chuo Kikuu cha Kisangani (UNIKIS) na wenyeji kwa washirika wa kimataifa na kitaifa kutekeleza FCCC. Washiriki wakiwemo Resources and Synergies Development (RSD) ambayo inaratibu mradi huo na pia Virunga Foundation, na World Agroforestry Centre (ICRAF), WWF, Chuo Kikuu cha Gembloux na *Jardin Botanique de Meise*. Mradi wa miezi 47 ulizinduliwa mwezi Februari 2013.

Lengo kuu ni kusaidia kukuza uwezo wa DRC na kutumia juhudi za tafiti kupunguza ukataji miti na uharibifu wa misitu na hivyo kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Mradi wa FCCC unajumuisha nadharia na vitendo. Hususani inafanya kazi ili:

1. Kujenga uwezo wa tafiti kwenye mabadiliko ya tabia nchi na misitu kwa UNIKIS katika jimbo la Oriental, Chuo Kikuu cha Goma na Chuo Kikuu Katoliki cha Graben huko Butembo, Kivu Kaskazini na Chuo Kikuu cha Bukavu cha Jimbo la Kivu Kusini.
2. Kuchochea maendeleo ya mashamba na kilimo mseto nje ya Hifadhi ya Taifa ya Virunga na kurejesha ardhi na misitu iliyoharibika ndani ya mipaka yake na hivyo kupunguza msukumo kwenye Hifadhi yenyewe.

## 1. Kujenga uwezo wa kitaaluma na tafiti katika misitu

Utafiti wa uwezo wa tafiti za misitu nchini DRC wa mwaka 2005 ulibaini uhaba mkubwa wa wataalamu wenye uwezo na kufuzu kitaaluma katika nchi ambayo inategemea sana rasilimali zake za misitu.

Kuna wanasayansi wachache wenye ari na wenye shahada za Uzamili (MSc) na Uzamivu (PhD) iwe katika MECNT au taasisi nyingine DRC ikiwemo *L' Institut pour l' Etude na la recherche agronomiques* (INERA). Ni wazi kwamba kulikuwa na hitaji la kuongeza uwezo wa kitafiti endapo rasilimali za misitu ya nchi ihifadhiwe na isimamiwe kiuendelevu katika siku zijazo.

Tangu mwaka 2009, kwa ruzuku toka Umoja wa Ulaya, CIFOR imeendesha mradi wa REFORCO (*Appui à la recherche forestière au Congo*) ambao ulihusisha ufadhili kwa wanafunzi wengi wa shahada ya Uzamili (MSc) na Uzamivu (PhD) katika eneo la misitu kwenye chuo cha UNIKIS.

FCCC imeongeza mafanikio ya REFORCO kwa kuwezesha zaidi wanafunzi wa Kikongo wa shahada za uzamili (MSc) 42 na uzamivu (PhD) 11 kubobea katika masuala ya mabadiliko ya tabia nchi, usimamizi endelevu wa misitu na utawala kwa kushirikiana na vyuo vikuu ya Kisangani, Goma, Graben na Bukavu.

Mradi unaendelea kuwezesha wanafunzi 13 wa Uzamivu (PhD) toka REFORCO. Miradi ya utafiti inahusiana na programu ya Taifa ya DRC ya Misitu na Vipaumbele vya Tafiti na mtaala unaoanishwa na mipango ya serikali ya kuwa na elimu ya juu sawa kwa nchi nzima.

Mradi wa FCCC una vitengo vya uratibu vinavyoongozwa na RSD Kinshasa, Kisangani na Goma sambamba na wanasayansi wawili wa CIFOR wanaofanya kazi katika mradi huo; mmoja katika Chuo Kikuu cha Kisangani na mwingine akiwa Goma ili kusaidia wadau wote wanaofanyakazi katika Mashariki ya DRC.



Kuongezeka kwa uwezo wa tafiti za misitu nchini DRC ni muhimu kwa watumiaji wa misitu nchini humo. Picha na Olliver Girard/CIFOR



Wanafunzi wa masuala ya misitu katika Chuo Kikuu Kisangani wakiwa nje ya jingo la bluu kwenye kampasi lililokarabatiwa chini ya mradi wa CIFOR-REFORCO. Kwenye tukio la CIFOR la Mkutano wa kwanza wa Kimataifa juu ya viumbe anuai ndani ya Bonde la Kongo. Picha na Joan Baxter/CIFOR




Democratic Republic of Congo

Zaidi ya uwekezaji huu katika maendeleo ya rasilimali watu, mradi unatoa msaada mkubwa katika miundo mbinu kwa ajili ya kusaidia UNIKIS yenyewe. Hii ni pamoja na msaada kwa ajili ya ukarabati wa madarasa, kumbi za mihadhara na ofisi, vifaa vya teknolojia ya mawasiliano, vifaa vya kutumika katika tafiti za misitu, na kuleta upatikanaji wa mtandao wa intaneti katika kampasi za vyuo vikuu. Wanasayansi wote wa CIFOR walio DRC na wale wanaotembelea toka majimbo mengine wametengeneza mitaala inayohusiana na mambo ya misitu na wanafundisha kozi za chuo kikuu.

## 2. Kupunguza utegemezi kwenye Hifadhi ya Taifa ya Virunga kwa miti katika uwanda

Lengo kubwa la pili la mradi wa FCCC ni kusaidia usimamizi endelevu na uadilifu wa kutunza mazingira yenye mchanganyiko wa kipekee wa kibaiolojia wa Hifadhi ya Taifa ya Virunga na uwanda wa jimbo la Kivu Kaskazini.

Virunga, hifadhi kongwe katika Afrika na Eneo la hifadhi ya kale la kidunia (UNESCO) na ipo katika hatari kubwa ya kuharibiwa. Vita ya wenyewe kwa wenyewe na mauaji ya kimbari ya Rwanda yamesababisha ongezeko la wakimbizi jambo ambalo limesababisha ongekezo kubwa la mahitaji ya kuni na mkaa ambacha ni chanzo kikuu cha nishati katika kaya kwenye ukanda huo. Sehemu kubwa ya hayo hupatikana toka katika misitu ya milimani iliyo ndani na kwenye mipaka ya hifadhi na kusababisha ukataji miti na uharibifu wa mazingira.

Katika jitihada za kukabiliana na hali hii na kupunguza msukumo kwenye hifadhi, CIFOR imeshirikiana na WWF kunzisha programu ya upandaji miti kwa kushirikiana na wakulima wa ndani ili kukidhi mahitaji yao na kupunguza msukumo wa kilimo kwenye misitu ya hifadhi.

ICRAF inawezesha tafiti ili kutengeneza chaguo za kilimo mseto mahsusi katika kuongeza uzalishaji mwingi wa huduma za mfumo wa kiikolojia ikiwemo kuongeza viumbe anuai na upatikanaji wa masoko kwa wakulima wa ndani.

CIFOR ina ratibu tafiti katika masuala ya; upimaji kiasi cha ujazo wa misitu, fedha kwa ajili ya hewa ukaa, kuboresha maisha ya viijijini na utawala bora wa misitu.

Mradi pia unalenga kuanzisha na kuboresha mfumo wa kilimo mseto na mashamba makubwa kwenye ekari 3,000 nje ya Hifadhi ya Taifa ya Virunga na kushirikiana na Virunga Foundation/*Insitut Congolais pour la Conservartion de la Nature* (ICCN) ili kurejesha ekari 5,000 za ardhi iliyoharibiwa ndani ya hifadhi.



Sokwe motto katika Hifadhi ya Taifa ya Virunga. Picha na Emilie Smith Dumont/ICRAF

## Matokeo mpaka kupata athari

Mradi wa FCCC unahimiza mawasiliano ya matokeo ya tafiti zake kama kipengele muhimu sana. Mwishowe, inatazamia kutoa makala za filamu kwa lengo la kuzitangaza, kutoa vitabu vya maelekezo na miongozo ya kiufundi na itahakikisha kwamba matokeo ya tafiti zake ikiwemo makala za kisayansi, tasnifu za Uzamili (MSc) na Uzamivu (PhD) zitatafsiriwa katika vipeperushi vya taarifa na Muhtasari wa sera na kusambazwa kwa kiasi kikubwa katika warsha na mikutano na kwa kupitia vyombo vya habari vya ndani na vya kimataifa. Idara ya Mawasiliano ya CIFOR inafanya kazi kwa ukaribu na mradi ili kuhakikisha matokeo yanaleta athari kwa watunga sera, watumiaji wa misitu na washiriki wengine.

## Kwa taarifa zaidi:

**Dr D. Andrew Wardell**

**CIFOR, s / c Biens et Services des Ecosystèmes Forestiers tropicaux (B & SEF)**

Kitengo cha Mazingira cha Sociétés du CIRAD TA C- 105 / D
34398 Montpellier Cedex 5, Ufaransa
Baruapepe: a.wardell@cgiar.org
Simu: +33 (0) 786 98 514 5

**Quentin Ducenne (PhD, MBA)**

**RSD,**

Baruapepe: fccc.coordination@gmail.com
Simu: +243 99 103 94 94

RESEARCH PROGRAM ON Forests, Trees and Agroforestry

Utafiti huu ulifanywa na CIFOR kama sehemu ya Programu ya CGIAR kwenye Utafiti juu ya Misitu, Miti na Kilimo Mseto (CRP - FTA). Mpango huu wa kushirikiano unalenga kuongeza usimamizi na matumizi ya misitu, Kilimo Mseto na rasilimali za kiasili za misitu katika uwanda mzima toka kwenye misitu hadi kwenye mashamba. CIFOR inaongoza CRP-FTA kwa kushirikiana na Bioversity International, CATIE, CIRAD, The International Center for Tropical Agriculture and the World Agroforestry Centre.





GCCA Global Climate Change Alliance

CGIAR Fund

cifor.org

**Kituo cha Kimataifa kwa Utafiti wa Misitu (CIFOR)**
CIFOR inastawisha maendeleo ya binadamu, utunzaji wa mazingira na usawa kwa kufanya tafiti ili kusaidia utengezaji wa sera na matendo yanayoathiri misitu katika nchi zinazoendelea. CIFOR ni mwanachama wa CGIAR Consortium. Makao makuu yetu yapo Bogor, Indonesia na ina ofisi Asia, Afrika na Amerika ya Kusini.